MUHAMMAD AL-TAHIR IBN ASHUR

# Ibn ASHUR

## Makala Kuhusu Makusudio ya Kisheria

SWAHILI VERSION

Idara ya Lugha na Ukalimani ya Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro

IIIT — Mfululizo wa Vitabu kwa Muhtasari

# Ibn ASHUR

## Makala Kuhusu Makusudio ya Kisheria

**SWAHILI VERSION**

Idara ya Lugha na Ukalimani ya Chuo Kikuu
cha Waislamu cha Morogoro

©International Institute of Islamic Thought, 2013

International Institute of Islamic Thought (IIIT)
P.O.Box 669
Herndon, VA 20172, USA
www.iiit.org

Toleo Halisi Limetafsiriwa Kutoka katika Kiarabu na Kilifafanuliwa na Mohamed El-Tahir El-Mesawi Kilifupishwa na Alison Lake.

Hakimiliki ya Kitabu hiki imehifadhiwa. Hairuhusiwi kukipiga chapa, kwa namna yoyote ile bila ruhusa ya maandishi ya wachapaji.
Rai na maoni yaliyo elezwa katika kitabu hiki ni ya mwandishi, na si lazima yatangamane na yale ya wachapaji.

Kimetafsiriwa na:

Tawaqal Juma Hussein

Kimehaririwa na:

Abdallah Suleiman Hamad

Design and layout by:

Iddi Suleiman Kikong'ona (iddkiko@ymail.com)

# MFULULIZO WA MUHTASARI WA VITABU VYA IIIT

Makala ya Ibn Ashur juu ya Makusudio ya Sheria ya Kiislamu (tafsiri ya Kingereza kutoka toleo la kwanza la Kiarabu) ilichapishwa katika ukamilifu wake mwaka 2006. Katika kazi hii mwanazuoni mashuhuri wa Kiislamu Sheikh Muhammad Al-Tahir Ibn Ashur amependekeza Maqaasiid as-shar'iyyah kama mbinu ya kuhuisha nadharia ya Sheria ya Kiislamu, ambayo bado haijaendelezwa sana tangu kipindi cha maimamu wakubwa.

Ibn Ashur alithubutu vilevile kuzungumzia mada nyeti ya makusudio ya Mtume Muhammad (s.a.w) katika vitendo vyake na maamuzi yake. Alianzisha vigezo vya kutofautisha juu ya hadithi za Mtume ambazo zimekuja kama sehemu ya Sheria ya Kiislamu na vitendo na maneno ya Mtume yanayokusudiwa kuwa na malengo maalumu kama vile uongozi wa kisiasa, hukumu za mahakama, ushauri wa kirafiki, utatuzi wa migogoro, n.k. Lakini mchango muhimu kuliko yote katika kitabu hiki ni kukuza Makusudio mapya kwa kuunda istilahi mpya ambazo zilikuwa bado hazijaundwa katika misingi ya zamani ya Fiqh. Kwa mfano, Ibn Ashur alianzisha nadharia ya kuhifadhi nasaba kwenda katika mfumo wa kuhifadhi na kulinda familia, nadharia ya kulinda itikadi ya kweli kwenda katika uhuru wa kuamini, n.k. Vile vile alianzisha dhana za kufanya vitu kwa utaratibu mzuri, silka za asili, uhuru, haki, unyenyekevu na usawa kama Makusudio katika haki zao; ambapo Sheria ya Kiislamu imeasisiwa katika misingi hiyo. Maendeleo

haya yanatoa fursa kubwa kwa Sheria ya Kiislamu kutatua matatizo ya wakati huu na changamoto halisi kwa makundi yote ya walio wengi na walio wachache ya jamii za Kiislamu.

Toleo lililofupishwa kutoka toleo halisi la Ibn Ashur

Makala ya Ibn Ashur Juu ya Makusudio ya Sheria ya Kiislamu

Imetafsiriwa na Mohamed El-Tahir El-Mesawi

ISBN hbk: 978-1-56564-423-9

ISBN pbk: 978-1-56564-422-0

2006

Yaliyomo

**NENO LA AWALI**

*Mfululizo Wa Muhtasari Wa Vitabu Vya IIIT iii*

**UTANGULIZI 1**

**DIBAJI**

*Uzushi Katika Mila za Kiutume:*

*Sababu Zake na Hatua za Kuzirekebisha 3*

**SEHEMU YA KWANZA**

*Uanzishwaji wa Makusudio ya Shari'ah 5*

**SEHEMU YA PILI**

*Makusudio ya Jumla ya Sheria ya Kiislamu 11*

**SEHEMU YA TATU**

*Malengo ya Shari'ah:*

*Miamala Ya Kibinadamu 25*

**HITIMISHO 30**

# UTANGULIZI



**Ibn Ashur** (Muhammad Al-Tahir) ni Sheikh na Imamu maarufu kutoka katika nchi ya Tunisia na ni mmoja miongoni mwa wanazuoni wakubwa na maarufu wa Kiislamu wa karne ya 21. Kitabu hiki "Makusudio ya Sheria ya Kiislamu" ni miongoni mwa kazi muhimu kabisa katika masomo ya Sheria ya Kiislamu (Shari'ah) zilizoandikwa kwa lugha ya Kingereza. Ibn Ashur alipendekeza Makusudio ya Shari'ah kama mbinu ya kuhuisha nadharia ya Sheria ya Kiislamu ambayo kwa hakika bado haijaendelezwa sana tangu kipindi cha maimamu wakuu wa Fiqh; kutoka katika kipindi cha Al-Shafii wa karne ya nane hadi Shatwibii wa karne ya 14. Ibn Ashur alitumia mbinu ya kati baina ya misimamo miwili mikuu inayokinzana: msimamo mmoja unajulikana kama; 'siyo bunifu mpya,' Huu ni msimamo ambao hupuuza na hautilii maanani razini "isiyo mantiki" na ufasiri mpya wa hukumu za Shari'ah ili ziendane na mitazamo halisi ya utamaduni wa Waislamu. Msimamo wa pili unajulikana kama 'falsafa mantiki mpya,' ambao hupuuza utambulisho wa kidini na kitamaduni wa Waislamu katika kitu chao cha kwenda na wakati na kutafuta uwiano.

Makusudio ya Shari'ah ya Kiislamu msingi wake ni maandiko na Imani ya Kiislamu na huwa yanabainisha razini, malengo, na uzuri wa hukumu za Kiislamu. Vile vile Ibn Ashur alizungumzia mada nyeti ya dhamira au malengo yaliyopo nyuma ya matendo na maamuzi ya Mtume Muhammad Swalla Allahu 'Alayhi Wasallama. Ibn Ashur alianzisha

vigezo vya kutofautisha kati ya hadithi za Mtume Swalla Allahu 'Alayhi Wasallama zinazohusiana na mambo ya Sheria ya Kiislamu (Shari'ah) na yale matendo ya Mtume Swalla Allahu 'Alayhi Wasallama yasiyohusu mambo ya Kisheria pamoja na maneno yake yenye makusudio mengine maalumu. Mchango muhimu wa kitabu hiki uko katika kukuza Makusudio ya Shari'ah pamoja na istilahi ya kisasa kazi ambayo ilikuwa bado haijafanywa katika Misingi ya Fiqh (Usul-Fiqh). Michango ya Ibn Ashur kwa ujumla ilifungua fursa kwa Sheria ya Kiislamu kuzungumzia changamoto za kisasa na halisi kwa jamii ya Kiislamu na kwa makundi machache ya Waislamu.

Muhammad Al-Tahir Ibn Ashur alizaliwa nchini Tunisia mnamo mwaka 1879 katika familia ya kisomi yenye asili ya Kihispania. Alisoma kwa moyo wa kutaka kuleta mageuzi ya kifikra na vile vile aliweza kumudu vizuri taaluma za kale za Uislamu. Alichaguliwa kuwa hakimu na kisha akapata cheo miongoni mwa vyeo vikubwa katika Uislamu yaani cheo cha Sheikh wa Uislamu "Shaikh al-Islaam" mwaka 1932. Ibn Ashur alikuwa mwandishi mahiri na mtunzi katika fani ya kuleta mageuzi katika taaluma ya Kiislamu na fiqh. Kazi aliyofanya Ibn Ashur mwaka 1946 kuhusiana na Makusudio ya Sheria ya Kiislamu inachukuliwa kuwa mchango mkubwa katika nyanja ya kujifunza Makusudio makubwa ya Shari'ah.

# DIBAJI

*Uzushi Katika Mila za Kiutume:*

*Sababu Zake na Hatua za Kuzirekebisha*



Kitabu hiki kinakuza mjadala muhimu katika Makusudio ya Shari'ah katika kutoa mwongozo na rejea wakati wa kuzungumzia tofauti za rai. Kitabu kinalenga kuwasaidia Waislamu kupata tiba ya kisheria kwa mambo yao muhimu hasa pale yanapotokea mambo mapya na kuwapa rai ya mwisho pale wanapokabiliana na hoja zinazokinzana za madhehebu mbalimbali.

Tofauti juu ya kanuni za msingi (Usul) huendelea kuwepo kuhusiana na hukumu zilizotumika kwa sababu kanuni za ujumla na kanuni kuu za Misingi ya Fiqh (Usul-Fiqh) zinatokana na sifa maalumu za hukumu hizo.

Misingi ya Fiqh (Usul al Fiqh) haijawahi kuwa msuluhishi wa mwisho ambaye Fat'wa yake inakubalika na wale wanaopingana juu ya mambo ya kifiqh. Zaidi ya hapo maazimio na maswali mengi ya Usul al Fiqh ni mara chache hutimiza lengo la kuelezea hekima na kuanzisha malengo hayo. Hivyo, wanazuoni wa Misingi ya Fiqh wameelekeza maswali yao kwa sura za nje na istilahi za kilugha za Shari'ah. Tunahusika zaidi na kupima hali halisi ya makusudio halisi ya Usul al Fiqh.

Kuleta kanuni bora na dhahiri kwa ajili ya kuifahamu vizuri Shari'ah, tunahitaji kurudi katika makusudio ya asili ya misingi ya fiqh

inayokubalika kiasili pamoja na kuyaunda upya. Kisha kuiunda upya fani yote ya Usul al Fiqh na kuiweka kama taaluma yenye kujitegemea inayoitwa "Sayansi ya Malengo Makuu ya Shari'ah." Kitabu hiki kinaelezea Makusudio ya Uislamu yanayohusu Sheria na hukumu zinazohusu miamala na tabia. Sheria hizi zinastahiki kuitwa Sheria za Kiislamu kwani zinaakisi wazi lengo la Uislamu la kubainisha na kutambulisha viwango mbalimbali vya manufaa na madhara na vigezo vya kuzipimia.

# SEHEMU YA KWANZA

## *Uanzishwaji wa Makusudio ya Shari'ah*



Katika sehemu hii tunakusudia kuthibitisha kuwa Sheria ya Kiislamu (Shari'ah) kwa ujumla wake imeyakusudia malengo makubwa na pia kuthibitisha kwa nini mwanazuoni wa fiqh ni lazima ayajue, pamoja na aina za malengo, na njia za kuyachanganua na kuyathibitisha. Hukumu na Sheria za sheria yoyote ile tukufu zimewekwa kwa ajili ya mwanadamu na huwa zinalenga makusudio fulani ambayo Mwenyezi Mungu ameyakusudia. Allah aliwatuma Mitume na akateremsha sheria ili kuweka mfumo wa kibinadamu. Zaidi ya hapo, wanadamu humiliki silka waliyopewa na Muumba kwa ajili ya ustaarabu wao ambayo alama kubwa kabisa ya silka hiyo ni kutunga sheria kwa ajili ya kurekebishia maisha yao. Unapoipima Qur'an tukufu na Hadithi sahihi za Mtume unaweza kukata shauri kuwa hukumu za Sheria ya Kiislamu zimejengwa katika sababu za ndani ambazo huzunguka katika suala zima la kuleta manufaa kwa watu wote na kuinufaisha jamii na watu wote kwa ujumla.

Mwanazuoni wa Fiqh anahitaji kujua malengo ya Sheria ya Kiislamu katika viwango vifuatavyo:

Moja: Anatakiwa kufahamu maelezo na maana yake kwa kutumia kanuni za kilugha zinazotawala hoja za kifiqh zinazoelezwa katika misingi ya Fiqh. Vile vile anahitaji kufahamu khitilafu kwa kutumia viashiria au vipimo vilivyowekwa na mujtahid, na zaidi achunguze malengo na

hukumu za Shari'ah. Kutohoa hukumu za Shari'ah kwa kutumia Qiyasi kunategemea uhakiki wa sababu husika na hili linahitajia mtu kuwa na taaluma ya Makusudio ya Shari'ah. Malengo ya juu ya Shari'ah ni miongoni mwa vigezo vinavyotumika katika kupimia usahihi wa Hadithi za Mtume (s.a.w), kuzingatia na kuyafanyia kazi mawazo ya wataalamu wa Fiqh: miongoni mwa maswahaba na wanazuoni wa mwanzo, na ni njia mojawapo ya kuzikubali hoja na sababu za kifiqh.

## Njia za Uanzishaji Malengo ya Shari'ah

Sheria ya Kiislamu ina malengo makubwa katika hukumu zake kwa mujibu wa ushahidi, dalili na hoja zake. Makusudio mbalimbali ya Sheria ya Kiislamu ambayo yamejengeka katika hoja za misingi ya Fiqh zilizoeleka. Ingawa hoja hizi zinachukuliwa kutoka katika Qur'an tukufu ambayo aya zake hazina shaka na zimepokelewa kwa msingi wa tawaatur au kupokelewa na idadi kubwa ya wapokeaji; lakini viashiria vyake vingi haviko katika hukumu ya wazi au moja kwa moja. Ndio maana Mujtahiduna wamekhitalifiana kuhusiana na hukumu na sheria mbalimbali wanazotohoa kutoka katika Qur'an.

Kanuni kubwa kuliko zote za mwanazuoni wa Fiqh katika hali hii ni kushikamana na lengo na uadilifu na kuachana na kuegemea au kumili katika hukumu iliyotolewa au kumili katika rai ya Ijtihadi iliyopita au uoni wa mwalimu au mwanazuoni mkubwa. Njia muhimu ya kufikia hitimisho la msingi la Malengo ya Sheria ya Kiislamu inapatikana katika silka na vipimo mbalimbali. Tunapofanya uratibu wa jumla wa visababishi ambavyo vinashirikiana katika hekima moja tunaweza kutohoa lengo moja na hivyo kuhakiki lengo kusudiwa la Shari'ah.

Vile vile tunaweza kupima dalili zinazohusu amri na hukumu za Sheria ya Kiislamu ambazo zina sababu moja. Hapo tunaweza kuhitimisha kwa yakini pasi na shaka yoyote kuwa sababu hiyo ndiyo inayowakilisha kusudio la Mwenyezi Mungu. Kauli za wanazuoni waliotangulia zinabeba ushahidi wa wazi juu ya umuhimu wa kuzingatia Makusudio ya Shari'ah. Vile vile kauli zao nyingi zinaonesha kuwa walikuwa wanayatafuta malengo na makusudio ya Shari'ah katika matamko ya Kisheria kwa kupitia njia ya kutohoa. Usahihi zaidi wa rai za wanazuoni wakubwa au Mujitahidina unategemea undani na umakini wa juhudi zao katika kuyatafuta makusudio ya Shari'ah.

Muktadha wa mazungumzo ambao hujumuisha ushahidi wa dalili za Qur'an na Sunnah, hotuba zinazotolewa na muktadha wa mambo kwa ujumla wakati mwingine unaweza usifahamike au usieleweke na baadhi ya wanazuoni. Wanazuoni wa Fiqh hutofautiana waziwazi katika kuyazingatia haya. Hata hivyo ni wachache wanaoweza kueleza kwa kutumia njia ya uchunguzi wa kina wa matendo ya Mtume na silka zake. Hivyo mkazo ni lazima utolewe juu ya rai za maswahaba katika mambo ya Kifiqh kwa kutegemea ufikishaji wao na matendo yao. Kwa hiyo inapotokea wanazuoni wa fiqh kukabiliwa na aina mbalimbali za tafsiri, walikuwa wanauliza ufafanuzi wake kutoka kwa Mtume wa Allah, kama vile walivyokuwa wakichunguza matukio ambayo yangeweza kuwapa uoni juu ya Makusudio ya Allah katika mambo mbalimbali.

## Lengo la Mtume Kuweka Sheria

Ni stadi muhimu kwa anayejifunza au anayetafuta makusudio ya Shari'ah kutofautisha malengo tofauti kati ya maneno na matendo ya Mtume. Mwanachuoni Shihaab al-Qaraaf alikuwa ndiye mwanachuoni wa kwanza kuidiriki na kuifanyia kazi tofauti hii. Katika hili aliandika hivi: "Mtume wa Allah ndiye kiongozi mkuu, hakimu mweledi na mwadilifu zaidi na ndiye hakimu mwenye ujuzi zaidi kuliko wanadamu wengine… Hatuwezi kufikiria juu ya jambo lolote lile la Kiislamu pasi na kumfikiria Mtume kama kiigizo chema kwetu…" Akaendelea kusema kuwa: "…matendo na tabia zake katika nafasi zilizotajwa hapo juu yana athari tofauti katika Shari'ah. Kwa hiyo kila kitu alichosema Mtume au alichofanya kwa njia ya kupelekea na kufikishia watu ni Shari'ah au kanuni inayolazimu kutekelezwa…"

Maswahaba wa Mtume walitofautisha wazi kati ya amri za Mtume zilizotoka kwake ambazo zilikuwa katika mfumo wa Sheria na zile ambazo hazikuwa katika mfumo huo. Maelezo au vitendo vya Mtume katika nafasi zifuatazo: Sheria, Fat'wa, usuluhisho, uongozi wa nchi kisiasa, mwongozo, ushauri kwa wale waliokuwa wakihitaji rai yake, ushauri nasaha, kuamsha na kuhamasisha nyoyo, kufundisha umuhimu wa kujipamba na sifa ya ukweli, kuadabisha, na matamko yake ya kawaida yasiyokuwa ya kimaagizo. Nafasi zote hizi ni dalili za wazi za Sheria ya Kiislamu na zinatofautiana kutokana na aina za hukumu za Shari'ah zinazozihusu.

Kutoa Fat'wa na haki ni mifano ya matumizi ya Shari'ah. Nafasi ya uongozi mkuu wa dola katika hali zote inatakiwa isichanganywe na zile zinazohusu nafasi ya Shari'ah. Nafasi ya mwongozo na maelekezo ni ya ujumla zaidi kuliko nafasi ya Sheria kwa sababu Mtume wa Allah anaweza kuamrisha na kukataza wakati nia yake sio ya moja kwa moja, bali anaweza kufanya hivyo ili tu kuonesha njia tofauti za kuliendea jambo zuri na la sawa.

Mwanachuoni wa Fiqh anatakiwa achunguze kwa kina mazingira na ushahidi wa kimazingira wa matendo mbalimbali ya Mtume. Viashiria vya kimuktadha vinavyohusiana na Shari'ah vinajumuisha kuhusika kwa Mtume katika kutoa maneno yake kwa Umati wake, kutekeleza kwake kwa dhati kivitendo yale yote aliyoyasema, na kuunda amri za Kishari'ah  katika mfumo unaowahusu watu wote.

## Malengo ya Shari'ah Halisi na Dhahania

Makosa ya Kifiqh yana athari mbaya kwa mtu na jamii kwa ujumla. Wanazuoni wanaasa lisipimwe lengo lolote lile la Shari'ah kabla ya kusoma kwa undani silka zinazohusu aina ya mafundisho mbalimbali yanayohusu malengo ya Kishari'ah , na kabla ya kupitia kwa kina kazi za wanazuoni wa Fiqh kwa ajili ya kupata ufahamu sahihi.



Mchakato mzuri wa kuhakiki malengo ya Shari'ah na kupima mambo kwa undani wake ni muhimu sana katika suala zima la kuepuka kukosea. Maarifa au elimu aliyopata mtafiti wa malengo ya Shari'ah vinaweza kuonekana katika sura mbalimbali: yakinifu, dhahania sana au dhahania kidogo. Wanazuoni wa Fiqh wanatakiwa waainishe idadi kadhaa za malengo makuu yenye ubora timilifu na yenye hukumu ya moja kwa moja kama rejea na vigezo vya mwisho katika mambo mbalimbali ya Kifiqh.

Lengo ni kuunda seti ya kanuni za moja kwa moja na zenye mashiko ya wazi ya Kishari'ah  ambazo zitakuwa kama fremu itakayotumika kama rejea pale panapokuwa na hali ya kutokubaliana au panapokuwa na ukaidi, kutoa elimu ya makusudio ya Shari'ah yanapotofautiana na misingi ya Fiqh. Malengo dhahanifu yanaweza kupatikana kwa urahisi kupitia uanzishwaji wa kanuni za mwongozo juu ya hukumu za Shari'ah. Utohoaji wa sawa wa hukumu za Kiislamu utawapeleka wanazuoni

kusema wazi kuwa kuhimiza wepesi ni moja kati ya malengo makuu ya Sheria ya Kiislamu.

Viashiria vyote vilivyochunguzwa kwa utafiti wa msingi wa utafiti wa kina hurejea rejea, vina sifa ya ujumla na vinapatikana katika dalili za Qur'an zenye maana ya wazi na ya moja kwa moja. Viwango vya dhana katika kuyaelewa makusudio ya Shari'ah vinategemea viwango tofauti vya ufuatiliaji, umuhimu wa vyanzo na viashiria vyake vilivyowekwa na wanazuoni wa Fiqh wanaofanya utafiti wa viashiria hivyo.

## Maamrisho ya Shari'ah Yanayotambulika na Yasiyotambulika Kwa kutumia Akili

Utaratibu ulioanzishwa na wanazuoni wa Fiqh kwa ajili ya kufikiri na kujenga hoja katika Fiqh na misingi yake umejikita juu ya maana ya kilugha ya matamshi ya Qur'an, maneno ya Mtume, matendo yake na kusudio lake pale aliponyamaza. Kauli hizo zinaweza kuashiria hukumu na sheria zinazowahusu watu wote. Wanazuoni wa Fiqh wametohoa hukumu mbalimbali maalumu kwa kutumia kigezo cha visababishi vya kanuni za ujumla na kwa kutumia njia ya Kipimo au Qiyas kwa hukumu maalumu.

Baada ya kutumia juhudi zote zinazowezekana na kushindwa kugundua makusudio maalumu ya Allah katika hukumu fulani, mwanachuoni mwenye kujitahidi au mujtahid hufikia hitimisho la kuwa Shari'ah inatutaka tujisalimishe kwa maamrisho ya Allah kama sehemu ya Imani yetu. Wanazuoni wa Fiqh wanatoa hoja ya kuwa amri za Kishari'ah zinaweza kutambulika sababu zake kwa kutumia akili au haziwezi kutambulika kwa kutumia akili.

Wakati wanazuoni waliofikia daraja ya kufanya Ijtihad au mujtahiduna wanatofautiana katika zile hukumu ambazo haziwezi kutambulika kwa akili, wanazuoni ambao wamezungumzia suala la Qiyas wamegawa amri za Shari'ah katika makundi matatu: Zile ambazo zinatambulika wazi katika nususu na hoja za Kishari'ah ; zile ambazo ni amri za kiibada ambazo sababu zake ziko nje ya utambuzi wa mwanadamu kwa kutumia akili yake; na zile za kati na kati ambazo zina sababu ambazo wanazuoni wa Fiqhi wanaweza kuzitohoa kiakili ingawa wanaweza kutofautiana katika sababu zilizotoholewa. Wanazuoni wanapokuwa na

yakini kuwa amri fulani ni ya kiibada wanalazimika kuuhifadhi mfumo wake bila kuubadilisha. Wanazuoni wa Fiqhi hawana budi kuchunguza na kuchambua kwa makini zile Hadithi zenye sababu zilizojificha na makusudio yaliyojificha ili kupata njia iliyokuwa nzuri zaidi ya kupata lengo maalumu la Shari'ah. Vile vile wanatakikana wazingatie hali ya ujumla ya Ummah wa Kiislamu wakati zilipoSemwa Hadithi hizo. Tuna uhakika kuwa amri zote za Shari'ah zina makusudio ya Allah ndani yake ambayo yanajumuisha sababu, manufaa na maslahi.

# SEHEMU YA PILI

*Makusudio ya Jumla ya Sheria ya Kiislamu (Shari'ah)*



## Sifa Na Kigezo Kinachopima Makusudio

Makusudio ya jumla ya Sheria ya Kiislamu yanajumuisha maana pana zaidi na/au sura za ndani zaidi za hekima za Allah katika maeneo ya Shari'ah na hali zake. Makusudio hayo yanajumuisha tabia za jumla za Shari'ah. Makusudio ya Shari'ah yanaunda mawazo ya ujumla yanayokubalika na binadamu wote ambayo kimsingi ni lazima yawe yakinifu, wazi na yasiyobadilikabadilika. Mawazo ya ujumla yamepimwa kwa kigezo cha wakati, hivyo yanajulikana na yanakubalika na watu wote kutokana na kulandana kwake sanjari na mambo mazuri yanayokubalika na watu wote.

Baadhi ya mawazo yanaweza yasiwe na sifa ya kutobadilikabadilika na hivyo yakawa yenye kuyumbayumba kati ya uzuri na ubaya au manufaa na madhara. Katika hali hii hayawezi kukubalika moja kwa moja au kukataliwa moja kwa moja kama makusudio ya Shari'ah. Hivyo ni lazima yarejeshwe kwa wanazuoni na viongozi wa Ummah wa Kiislamu ambao ndio wenye mamlaka ya kuyaondoa au kuyabakisha. Mawazo hayo yanapokubalika kwa masharti yake, hivyo tutakuwa na yakini kuwa ni sehemu ya makusudio ya Shari'ah.

Itachukuliwa kuwa Allah kakusudia yafanyiwe kazi kila panapokuwa na fursa ya kuyafanyia kazi. Hivyo ni juu ya wanazuoni wa Fiqh kuyahakiki kama hali maalumu ambazo zinakaribiana na kanuni za jumla na hivyo hawatatakiwa kuyapeleka mbali zaidi ya umaalumu huo. Hata hivyo kama itaonekana kuwa yanajumuisha malengo kusudiwa ya kawaida ya Shari'ah, hapo wanazuoni wa Fiqh wanaweza wakayachukua na kuyapeleka mbali zaidi ya umaalumu wake.

Shari'ah haikubaliani na kujenga na kuasisi amri zake kindoto na kudhania. Ndoto na dhana ni jambo lisilokubalika Kishari'ah isipokuwa mpaka kuwe na dharura inayopelekea hivyo. Vitu vya kudhania tu au visivyokuwa halisi ingawa sio sawa kuvichukulia kama makusudio ya Shari'ah vinaweza kuwa na manufaa katika kupata baadhi ya makusudio ya Shari'ah kama vile kuwalingania watu katika Uislamu au kuhamasisha au kukhofisha kama njia ya kuhamasisha.

## Kujenga Msingi wa Makusudio ya Sheria ya Kiislamu katika Maumbile na Ukubwa wa Allah



Fitrah ni silka ya asili na mfumo ambao Allah kauweka katika kila kiumbe. Kwa hiyo fitrah ya wanadamu ni ile hali ya umbile lao la ndani na nje; akili na mwili. Vile vile kulinganisha athari na visababishi vyake. Hivyo kukata kauli juu ya jambo fulani kwa kutumia fitrah ni jambo linalokubalika kiakili kwani vitu visivyo vya kweli vinapingana na silka ya mwanadamu. Uislamu unajumuisha imani na Sheria; hivi vyote ni vitu vinavyotambuliwa na vinavyokubalika na akili. Shari'ah inawataka Waislamu kuihifadhi Fitrah yao na kuyahifadhi matendo yao yasiathiriwe na ustaarabu. Inapotokea mahitaji ya Fitrah yakawa yanakinzana na kuwa hayawezi kupatana, hapo kipaumbele kitapewa kile ambacho kinaonekana muhimu na kina nguvu zaidi katika kuihifadhi fitrah.

Kutumia Ada au "Urfu" au mazoea ya watu katika hukumu za Kishari'ah kunatokana na maana ya Fitrah Kishari'ah ambapo Fitrah ni sharti muhimu linalotumika kwa ajili ya lengo hili. Hivyo ada za watu hazitakiwi zipingane na kanuni za Shari'ah; la sivyo ada hizo hazitakubalika Kishari'ah.

Upole “Samaah” ni ule wepesi wa mtu mmoja kuamiliana na mwingine kwa huruma. Shari’ah imesimama kati ya ukali na upole. Hivyo “Samaah” inachukua maana yake kutoka katika dhana za upole, haki na uvumilivu. Upole ni sehemu muhimu au ndio msingi wa sifa zote njema. Upole unahimizwa katika mambo pale watu wanapoangukia katika ukali. Upole ni jambo jema ambalo halisababishi madhara au uharibifu. Qur’an na Sunnah zinathibitisha suala hili. Hekima yake ni kuwa Allah kaufanya Uislamu kuwa dini inayoendana na maumbile na silka ya mwanadamu. Kwa mantiki hiyo Shari’ah huleta huruma, wepesi na faraja kwa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla wake. Hili linaweza kuoneshwa wazi umuhimu wake mkubwa katika historia ya Sheria ya Kiislamu ilivyoenea pasi na kukatika. Na hili linahakiki zaidi kwamba wepesi ni jambo la kimaumbile (fitrah).

## Malengo ya Ujumla ya Sheria ya Kiislamu

Hukumu za jumla na dalili maalumu za Shari’ah zinaonesha kuwa kanuni ya lengo kuu la Shari’ah ni kuhifadhi mfumo wa jamii na watu na kuhakikisha ustawi wao. Dalili za wazi za Qur’an na Sunnah zinathibitisha kuwa lengo kuu la Shari’ah ni kuleta uadilifu na kuondoa dhulma katika aina zote za shughuli za mwanadamu.



Uadilifu unaokusudiwa na kusifiwa na Allah haujafungika katika uadilifu wa imani na ibada tu. Badala yake Sheria ya Kiislamu imeenda mbali zaidi na kuweka haki za watu katika hali ya maisha yao hapa duniani na mambo ya kijamii kwa kuzungumzia mambo ya mtu mmoja mmoja na jamiii na kuhuisha mambo yanayohusiana na imani na kuamini. Uislamu umezungumzia suala la kusafisha na kutwaharisha akili ya mwanadamu na kunyanyua nafsi ya mwanadamu.

Tangu mwanzo wa ulinganiaji wake, Mtume Muhammad Swalla Allahu ‘Alayhi Wasallama hadi baada ya kuhamia kwake Madina (Hijra), kidogo kidogo, Sheria ya Kiislamu iliweka mwongozo wa kutosha kuhusiana na mpango wa Shari’ah wa kuleta mageuzi yanayotakikana. Tunaangalia malengo maalumu ya kuleta mageuzi kwa mambo ya kijamii yanayohusu Waislamu katika hukumu na sheria zinazorekebisha mambo ya kijamii na miamala ya kijamii. Hii inajulikana katika Fiqh ya Kiislamu kama “Kuleta manufaa na kuondoa madhara”.

## Maslahi na Uharibifu katika Shari'ah

"Maslah" ni uadilifu wa juu kabisa na uzuri na sifa ya kitendo ambapo uadilifu na uzuri hupatikana mtu anapokuwa mbele ya watu au anapokuwa peke yake au anapokuwa faragha. Sifa hii ina faida muhimu kwa jamii au kwa mtu mmoja mmoja. "Mafsada" ni kinyume cha "Maslah" na ni sifa ya kitendo ambacho uharibifu na dhulma au madhara hutokea kwa mtu mmoja mmoja au jamii kwa ujumla wake. Maslahi ya jamii huhusu wajibu na majukumu ya pamoja ambayo hustawisha Umma. Maslahi ya mtu mmoja mmoja hunufaisha watu na yanahusu uadilifu na uzuri wa matendo ya mtu mmoja mmoja katika kuinufaisha jamii. Sehemu ya Sheria ya Qur'an na sehemu kubwa ya Sunnah zinahusiana na aina hii ya Maslahi.

Maelezo haya yanalenga kupata lengo muhimu na la jumla linalofariji wakati wa ugumu au mazito ili iwe ni utamaduni wa jamii na uwe ni utamaduni wa watu kuwasaidia wengine wakati wa matatizo na majanga na wawe tayari kuyakabili majanga. Ili kuhifadhi ustawi wa ulimwengu na uzima wa jamii, Shari'ah imeyazunguka maslahi muhimu ya mwanadamu na yasiyobadilika ambapo imeweka njia za kuyalinda hata katika hali ambazo inaonekana wazi kuwa hakuna manufaa. Kuweka maana ya wazi ambayo kupitia kwake sifa ya kitendo chochote itapimwa kama kitendo hicho kitachukuliwa kama Maslahi au Mafsada ni jambo nyeti linalohitaji maelezo makini na sahihi.

Ili kuzingatia kitendo chochote kile kuwa Maslahi au Mafsada; manufaa au madhara lazima yawe wazi, yaenee na yawe dhahiri kiasi watu wenye akili na busara wayatambue, sifa ya kitendo haiwezi kuchukuliwa na kitu kingine. Aidha katika kuleta manufaa au kubeba madhara. Moja kati ya sura za manufaa na madhara, ingawa iko sawa na kinyume chake, lazima iendane na kitu katika aina yake ambacho kinaifanya kiwe kizito zaidi ya sura nyingine; moja kati ya sura mbili za manufaa na madhara lazima iwe wazi na yakinifu, wakati nyingine si wazi na sio yakinifu.

Sheria ya Kiislamu daima inajumuisha malengo ya Maslahi na haileti Mafsada. Sheria hii inazuia Mafsada na hili halipelekei kuondoa Maslahi. Bali, Sheria ya Kiislamu kwa ujumla wake inalenga kufahamisha juu ya Maslahi. Mafsada ya moja kwa moja yanayozidi Maslahi hubadilika waziwazi kuhusiana na aina zake. Haya hayakubaliki Kisheria. Pamoja na tofauti zake zote, Maslahi ni ya aina kuu mbili: Aina moja inajumuisha

manufaa ya moja kwa moja kwa wanadamu. Haya Allah kayaweka katika silka ya asili ya mwanadamu na kuwa watu kwa maumbile yao hujikuta wakiyafanya na kuyahitaji kwa kuwa yanakubalika. Aina nyingine ya Maslahi hujumuisha manufaa ambayo hayako wazi sana. Shari'ah inahusika zaidi na kuondoa vizuizi vya kuyafikia manufaa ambayo hayako wazi zaidi. Maslahi ya manufaa yasiyo wazi sana yamekuwa yakibebwa kwa njia chanya na Sheria ya Kiislamu ambayo imeyafafanua vizuri na kuchagua adhabu maalumu kwa kuyatelekeza na kuyavunja.

Baadhi ya aina za Maslahi ya wazi yanaweza kujumuishwa chini ya ile aina ya Maslahi yasiyokuwa wazi zaidi kwa sababu ya kuwepo athari ambazo zinaathiri silka ya asili ya mwanadamu. Wale walioshikilia Shari'ah na wanaoweza kueleza kanuni zake za kisheria wanatakiwa kuzuia mikengeuko na mikinzano kwa ufundishaji utakaoondoa mawazo ya juu na mawazo haribifu. Inapotokea kuwa na mambo yasiyokuwa ya kawaida yanayomhusu mtu au watu fulani; suluhisho mwafaka zaidi ni elimu iliyokuwa nzuri na kuwakinaisha kiroho.

Ikiwa itakuwa kinyume na hivi, na ikawa wanavunja haki za watu wengine na kwa kufanya hivyo wakawa wanawadhuru kwa maneno au matendo; hapo suluhisho litakuwa adhabu. Shari'ah inafanya kazi katika mkakati wake kwa kulinda aina tofauti za Maslahi pamoja na kujizuia na kuvumilia, kutegemea na tathmini yake ya tabia za watu juu ya aina mbili za Maslahi. Shari'ah mara zote hulinda Maslahi yaliyodharauliwa na kutwezwa; yawe ni binafsi au ya kijamii, kama njia ya kulinda haki binafsi za watu na haki za jamii. Pale panapotokea mgogoro kati ya sura mbili tofauti za Maslahi kipaumbele kitapewa ile sura ambayo ni kubwa na muhimu kati ya sura hizo mbili. Shari'ah hutafuta kutambua malengo yake yanayohusu jamii yote pasi na kuleta ugumu na tabu kwa kupatanisha kwa kadiri iwezekanavyo sura tofauti za malengo yanayokusudiwa na maelezo na Sheria zake. Shari'ah hunyanyua jamii kutoka daraja ya chini hadi daraja za juu za malengo hayo kadiri hali zinavyoruhusu. Fitrah inaweza kutupa msingi wa kuunganisha kati ya hukumu za Shari'ah na hukumu zinazohusiana na mgogoro wa Maslahi na Mafsada na suala zima la kulinda asili ya mwanadamu isitwezwe.

Ifuatayo ni mifano ya mfanano wa aina za Maslahi ambazo Shari'ah inazichukulia na kuzizingatia na Mafsada ambayo huyaepuka. Wanafunzi wa makusudio ya Shari'ah wanaweza kujifunza na kugundua lengo la Allah na kufuata njia yake katika kuzungumzia Maslahi na

Mafsadi tofauti katika kukubaliana au kutokubaliana kutokana na hali ya jamii. Maarifa haya ni muhimu kuwa nayo kwa sababu Maslahi yako ya aina nyingi na yanatofautiana katika athari zake katika wema, ukweli na uzima wa jamii. Kwa hiyo yale Maslahi yanayojulikana ndiyo yanayochukuliwa na kuzingatiwa na Shari'ah. Maslahi yanaweza kugawanywa kutokana na athari zake na umuhimu wake juu ya uwepo wa watu na jamii. Lengo ni kufahamu aina mbalimbali za Maslahi kama zilivyokusudiwa na Shari'ah ili kupata maarifa kamili ya aina zake kwa ujumla.

Kisha tunaweza kuyagawa na kuyahukumu kwa mujibu wa kanuni zinazofaa. Shari'ah imeyaacha Maslahi yasiyo na dalili au zisizo na nguvu kama ni kanuni rejea. Maelezo ya Maslahi yanaweza kukabiliwa na dhana au kutokuwa kweli kwa mujibu wa dalili inaunga mkono aina tofauti za Qiyasi au kipimo kinachofaa, uainishaji wa sifa za kawaida, na usahihi wa ufanano ulioko kati ya asili na matawi mapya. Kwa upande mwingine ushahidi kwa ajili ya Maslahi ya ujumla unatokana na utohoaji na usomaji wa Shari'ah kwa kina ambao huleta ukweli juu ya mambo hayo.



Kufahamu wazo la Maslahi ndio njia ya wazi sana na ya moja kwa moja kwa wanazuoni wa Fiqh katika kushughulika na mambo ya jamii. Kama Maslahi yanapingana na yanatakikana yapimwe kutokana na kanuni zinazofaa ambazo zinahitaji hukumu inayojitegemea. Hukumu hii inabadilika kutokana na umuhimu wa vyote viwili; Maslahi yanayofuatwa na Maslahi yenye utata, vile vile katika kiwango cha ukweli kinachohusu uzito na nguvu zao.

## Kanuni za Jumla za Shari'ah

Sheria ya Kiislamu ambayo ni sheria ya mwisho iliyoteremshwa, ni kwa ajili ya walimwengu wote na hukumu na amri zake zinatumika sawasawa kwa watu wote kwa kadiri inavyowezekana. Allah ameiweka Sheria yake katika msingi wa hekima ya ndani na sababu za mambo ambazo zinaonekana, zinatambulika na hazibadiliki kwa dhana ya mataifa na ada za watu. Ingawa wanazuoni wa Kiislamu wanakubaliana kuwa Sheria ya Kiislamu ni kwa ajli ya ulimwengu wote lakini hawajaonesha ni kwa jinsi gani ufaaji huu unavyoonekana.

Kanuni kuu za Shari'ah, kanuni zake zinazohusu viumbe vyote, amri, na faradhi zake zinatumika katika mazingira yote pasi na ugumu au tabu. Hali za watu na mataifa katika nyakati mbalimbali zimekuwa bora pale wanapoyafanyia kazi mafundisho ya Uislamu pasi na ugumu wala tabu. Mifumo hii ya kufaa kwa Shari'ah imeungana na haiachani. Hekima na manufaa ya Shari'ah inaweza kuoneshwa katika hukumu mbalimbali ambazo kwa muundo ziko tofauti lakini zina lengo moja.

Moja ya athari muhimu kuliko zote za sifa ya kiulimwengu ya Shari'ah ni suala la usawa katika jamii. Hata hivyo, Shari'ah hukwepa kuweka usawa na mfanano katika kitu chochote ambacho hubadilika katika maumbile ya asili ya mwanadamu. Kama kuna mageuzi basi yameachwa yashughulikiwe na mifumo ya Kiislamu ya kijamii na kiraia kwa mujibu wa siasa za Uislamu badala ya kushughulikiwa na kanuni zake kuu za kisheria. Usawa wa binadamu ni jambo ambalo wamehakikishiwa watu wote katika Sheria ya Kiislamu. Ili kuanzisha usawa wa watu au vikundi katika Sheria ya Kiislamu hatutakiwi kutafuta sababu zake bali inatosha kuhakikisha hakuna kinachovunja usawa.



Vizuizi vya Usawa vinapelekea iwe muhimu kuakhirisha au kuondoa kabisa usawa kwa sababu ya Maslahi au Mafsada fulani yenye kutamalaki kutoka katika utendaji wake. Vizuizi hivyo vinachukuliwa kuwa vinatokea kwa bahati mbaya kutokana na athari yake ya kuakhirisha kanuni hii kuu ambayo ni ada katika Sheria ya Kiislamu. Vigezo vya kupima kiasi ambacho vizuizi hivi vinaweza kuondoa usawa kati ya wanadamu vinatoka katika uzingatiaji makini kwa akili safi au kanuni za Shari'ah.

Vizuizi vinavyozuia usawa katika maeneo fulani ya Shari'ah vinaweza kuwa vya asili na kuzaliwa navyo au vinaweza kuwa vya kisheria, vya kijamii au vya kisiasa. Mazingatio haya yanaweza kuwa ya muda au ya kudumu, yanaweza kuwa madogo au makubwa. Mazingatio ya asili, kisheria na kijamii yanahusiana na mwenendo wa kitabia, kuheshimu haki za watu wengine, na kusimamia vizuri shughuli za jamii ya Kiislamu kimfumo na kimaadili. Mazingatio ya kisiasa yanalenga katika kulinda nguvu ya kisiasa ya Kiislamu.

Shari'ah ni rejea na inaongoza katika kuainisha vizuizi hivi na kupima athari zake kwa kuzingatia kanuni zake maalumu ambazo utekelezaji wake kipaumbele chake kiko juu ya utambuzi wa usawa. Usawa katika

kuendesha mambo binafsi ni moja kati ya malengo ya asili ya Shari'ah. Neno la Kiarabu "hurriyyah" linamaanisha maana mbili; maana moja ikitoka katika maana nyingine. Maana ya kwanza ni kinyume cha utumwa na inamaanisha uwezo wa asili wa watu wote wenye ufahamu mzuri na waliokomaa kifikra kubeba na kusimamia mambo yao. Maaana ya pili inatoka katika maana ya kwanza kwa matumizi ya kinaya au majazi. Hii inamaanisha uwezo wa mtu kufanya jambo kwa uhuru pasi na kupata upinzani kutoka kwa mtu mwingine. Maana hizi mbili za uhuru zimekusudiwa na Shari'ah, kwani zote zinatoka katika fitrah na zinaakisi wazo la usawa.

Matumizi ya maana ya kwanza katika Shari'ah ni ya kawaida na yamejikita vizuri. Uzuri wa Shari'ah katika kutambua na kuyachukulia maanani maslahi ya jamii na maslahi shirikishi na kulinda mfumo wa kijamii umezuia isiondoe utumwa kwa mara moja (mkupuo mmoja), kutokana na kuwa na mizizi mirefu ya historia wakati wa kuja Mtume Muhammad Swalla Allahu 'Alayhi Waalihi Wasallama. Katika kuyatekeleza malengo yake, Uislamu ulilenga katika kuleta uwiano kati ya kueneza uhuru na kuhifadhi mfumo wa kijamii kwa kuhamasisha njia za kupata uhuru dhidi ya njia za kupata utumwa. Uislamu ulipiga vita visababishi na vyanzo vya utumwa na hivyo kupunguza idadi ya watumwa na kukomesha sababu nyingi zilizopelekea katika utumwa.

Uhuru wa kujieleza na kutafuta elimu vilionekana wazi katika karne tatu za mwanzo za Historia ya Uislamu wakati wanazuoni walipokuwa wanaweza kuelezea maoni yao na itikadi zao. Bila uhuru wa kujieleza, kukiri, mikataba, wajibu, talaka, na wasia na vinginevyo visingelikuwa na athari ya kisheria. Vitendo hivi visingekuwa na athari kama vingetokea kwa kulazimishwa. Uhuru wa kutenda ambao unaathiri watu wengine ni halali pale tu ambapo husababisha madhara. Katika sheria zake nyingi Shari'ah imelinda uhuru wa kutenda kwa kuziba njia zote zinazopelekea katika kuvunjwa au kuondoshwa uhuru huo.

## Malengo, Sifa Na Madhumuni Katika Shari'ah

Sheria ya Kiislamu imechukua mfumo mmoja wenye sura mbili zinazojumuisha kuondoa na kubakisha. Njia moja inajumuisha kuondoa dhulma na hii inamaanisha kuwabana watu na kutowapa uhuru wa kudhulumu, vile vile inamaanisha kumaliza kuchupa mipaka.

Sura moja ya badiliko lenye busara na lenye maana katika mambo ya mwanadamu ni kuchukua tahadhari katika kutekeleza pasipo kwenda kinyume, kwa kuwa kuachiwa huru hutishia kudhulumu pande zote mbili. Njia nyingine hujumuisha kukiri matendo mazuri ambayo yamefuatwa na wanadamu.

Kukiri kanuni ya kisheria ya ruhusa kunahitajika katika kumaliza kuchupa mipaka kwa watu wenye kuchupa mipaka kiitikadi kwa kuwahamasisha wafuate mfumo wa kati na kati ambao ndio mfumo wa kawaida na unakubalika na watu wengi wazuri na wenye fikra nzuri. Kukiri vile kunahitaji kuondoa fikra zozote potofu ambazo watu wanaweza kuwa nazo ambazo zinaweza kuwapelekea kuamini kuwa vitendo vizuri ni vibaya pale watu waovu wanapovifanya. Ukitoa sababu kama hizi na nyingine zifananazo, kunyamaza kwa Allah na Mtume Wake kwa jambo fulani kunachukuliwa kuwa wamekiri jambo hilo lifanywe na watu na kuwa ni zuri. Kwa hiyo ruhusa ni kanuni ya juu ya Shari'ah kuliko zote kwa sababu inajumuisha mambo mengi sana yasiyo na idadi.



Kubadili na kukiri ni vitu vinavyotumika kwa watu wote. Lengo la Shari'ah katika hukumu na maamrisho yake yote ni kuunganisha aina za hukumu hizo na amri, sifa, na matendo katika tabia ya mwanadamu au mwenendo wa mwanadamu mmoja mmoja au kwa pamoja. Uhusiano huu umejengwa katika maana muhimu za hali hizo, sifa, na matendo yanayopelekea katika wema na manufaa au ubaya na madhara. Ni hivyo hivyo mtu anatakiwa kuwa makini na imani potofu kuwa baadhi ya hukumu au kanuni na amri zinaunganishwa na majina ya vitu tu au kwa sura za nje pasipo kuzingatia maana za ndani na muhimu zilizokusudiwa na Shari'ah, kwa kufanya hivyo wakawa wanaangukia katika makosa mabaya ya kifiqh.

Istilahi za Sheria ya Kiislamu zinatakikana zitafsiriwe kwa mujibu wa maana zilizokusudiwa na Allah kuhusiana na matendo yaliyobebwa na istilahi za wakati ambapo istilahi za Kiislamu zilianzishwa. Pale ambapo kitendo kinapobadilika, istilahi inakosa thamani, bali kitendo ndicho kitazingatiwa. Kujifunza kwa kina Shari'ah ya Kiislamu na tabia zake ndiko kuliwaridhisha wanazuoni wa Ummah wa Kiislamu wazingatie vitu vingi vyenye sifa inayofanana kwa kuviweka chini ya hukumu moja kwa mujibu wa sifa zao shirikishi hata kama vina majina tofauti. Wanazuoni hutumia kanuni au hukumu za Shari'ah

zinazotawala matendo ya mwanzo kwa matendo ya baadaye kwa msingi wa sifa zilizoko nyuma ya sheria na wanapopitisha amri za Shari'ah. Umuhimu wa Qiyas kuhusiana na maana iliyokusudiwa na Allaha ni sahihi na wazi na unaambatana na mifano ya wazi. Kupigia mfano na kupima au Qiyas kwa wanazuoni ilikuwa muhimu katika kuweka wazi na kutambulisha maana nyeti na ukweli uliojificha. Mifano na Qiyas huwagharimu wanazuoni wa Fiqh juu ya juhudi ya kutafuta maana na aina za ndani zaidi.

Wanazuoni wakubwa wa Fiqh walitofautiana kuhusiana na matumizi ya Qiyas katika adhabu zilizo ainishwa bayana, kafara, na kusamehewa sababu, masharti na vizuizi. Hata hivyo baadhi ya watu wanaweza kutumia mbinu ya kugeuza muktadha wa Shari'ah kunakohusiana na matendo ambayo kukatazwa kwake ni ktika Sheria. Hii haijumuishi kutaka kufanya kitendo cha halali kwa njia tofauti au kwa kuweka njia za kuliendea. Imamu Bukhari alinakili Hadithi za Mtume zinazozungumzia tabasuri na akazigawa katika mfumo wa wanazuoni wa Fiqh, kwa mujibu wa vitendo tofauti vya wanadamu.

Katika tabasuri tofauti zilizotumika kukwepa amri za Shari'ah na hivyo kupelekea kuondosha sehemu ya malengo au malengo yote ya Shariah. Mbinu hii haifuati mtindo mmoja. Tabasuri katika vyanzo vya Shari'ah inaweza kufanya yafuatayo: kusababisha kuondolewa moja kwa moja kwa lengo la Shari'ah pasipo kulibadilisha na lingine; kuondosha kitendo halali na kuhamia kwenda katika kitendo kingine halali; kuondosha kitendo kimoja cha Kishari'ah ili kukiendea kitendo kingine cha Kishari'ah chepesi zaidi; kutumia vitendo ambavyo havina maana muhimu iliyokusudiwa na Allah na ambavyo havipingani na kusudio la Allah.

Kuondosha vitendo ambavyo vinaweza kusababisha madhara makubwa ambavyo kwa asili yake sio vibaya kunahusiana kwa ukaribu na sura ya mbinu ya kugeuza mambo. Hata hivyo baadhi ya watu wanatumia njia ya tabasuri ili waepuke baadhi ya amri za Kishari'ah. Wanaweza kufanya hivi ili kujenga sura na picha ya kuonesha kwa uwazi kuwa wanakubaliana na hukumu au kanuni za Shari'ah. Malengo ya Shari'ah yanalenga kuweka uwiano wa uzuri wa asili wa kitu ambacho kinatumika kama njia na madhara yake yanayowezekana kutokea. Kwa hiyo suala hili linaangukia katika hukumu inayotawala makinzano kati ya Maslahi na Mafsada.

Shari'ah inahusiana na njia zinazopelekea katika mambo mazuri na imeziruhusu kwa kuzijumuisha chini ya kanuni ya yale mambo ambayo ni lazima hata kama mwonekano wao rasmi unaweza kujumuisha kukatazwa kwao au kukubaliwa kwake. Hii inajulikana katika misingi ya Fiqh chini ya kanuni "kuwa kila kipelekeacho katika kitu kilicho wajibu nacho ni wajibu" na ni nija ya kulinda usalama wa jamii ya Kiislamu.

## Usahihi, Lengo, Mkazo na Huruma katika Sheria ya Kiislamu

Kwa kuwa Shari'ah imekusudia hukumu zake zinaweza kutekelezwa kwa urahisi na watu katika hali zote, vilevile imejumuisha usahihi na nguvu ya hoja ili kufanya maana zake ziweze kueleweka kwa uwazi. Vile vile imeweka sifa hizo kuwaonesha wanazuoni maana zilizoko nyuma ya Sheria. Wanazuoni wa Fiqh wanalenga juu ya sifa za wazi na dawama kama msingi wa hukumu na amri za Shari'ah. Vilevile wanakiri wazi kwamba kupatikana kwa sifa hizo kunaonesha maana iliyopo ambayo inaweza kuitwa hekima. Shari'ah hutumia njia hizi katika kufafanua kwa undani umuhimu na maana ili kuzuia mkanganyiko.

Shari'ah inakusudia amri na hukumu zake zitekelezwe na kufuatwa na jamii kwa sababu manufaa yake yaliyokusudiwa hayawezi kupatikana pasipo kutekelezwa kwa kanuni na hukumu zake. Ili kupata lengo hili, njia mbili zinatumika sawia. Moja ni matumizi ya ukali na utambulisho katika kutekeleza kanuni na hukumu zake. Nyingine ni matumizi ya wepesi na huruma kwa namna ambayo haiwezi kusababisha kuondoa malengo yake.

Shari'ah hutumia njia ya wepesi na rehma au huruma katika kuwahimiza watu kufanya kila lililo zuri kwao kwa kutekeleza hukumu zake. Hukumu za Shari'ah zimejengwa katika msingi wa wepesi wa kuzingatia hali za ujumla za wanadamu. Chini ya hali fulani Shari'ah hubadilisha hukumu na sheria zake kutoka katika ukali na ugumu kwenda katika wepesi na urahisi. Kwa hiyo kwa kufanya hivyo huwa inakifanya chepesi kile ambacho kingebeba shida na ugumu.

Shari'ah haitaki kuwabebesha wanadamu mizigo wasiyoweza kuibeba kwani ni sheria ya kivitendo ambayo inataka ufanyaji wa malengo ambayo yanaweza kupatikana tu kwa kutumia ukarimu. Kuepuka uzito

katika Shari'ah ni moja kati ya sifa kuu za Sheria ya Kiislamu. Uislamu unaporuhusu kitendo au unapolegeza Sheria yake huwa kwa hakika unaenda kwa mujibu wa sifa yake ya wazi ya upole.

Wanazuoni wa Fiqh wameondosha baadhi ya sura za ruhusa. Wanakubali kuwa ruhusa inajumuisha kubadili kitendo ambacho kimeamriwa kwa mtu mmoja au kwa jamii kutoka katika uzito kwenda katika wepesi kutokana na hali zinazolazimisha hivyo ambavyo zinaitaka Shari'ah kuacha lengo lake la kuleta manufaa na kuondoa madhara.

Hitajio kwa kawaida ni la jumla na la kudumu. Hii inajumuisha msingi wa Shari'ah inayohusu watu wote katika matendo yanayohusiana na aina za jumla za matendo ambayo awali yalikuwa yamekatazwa. Pamoja na kuwepo madhara yanayotokea kutokana na baadhi ya matendo na uwezekano wa kusababisha kwao hasara ya kifedha jambo ambalo linahitaji yakatazwe; lakini yameruhusiwa kwa sababu kubwa ya hitajio la jamii kwayo. Wanazuoni wa Fiqh wanatakiwa wazingatie umuhimu wa kudumu wa ujumla pale ambapo jamii yote au wengi wao watakuwa wanaweza kuwa katika hali inayohitajia ruhusa ya kitu kilichokatazwa ili kupata lengo maalumu na mahususi. Mkazo Kishari'ah unalazimisha mtu mwenyewe ajizuie kwa asili. Wanadamu kwa silka zao wanahitaji kupata baadhi ya manufaa au kuzuia baadhi ya mabaya. Kujizua kidini na kiroho na kukemea aina zote za mambo yasiyofaa sio jambo gumu kwa asili yake kwa mujibu wa silka na maumbile ya asili ya mwanadamu. Inapotokea kujizuia kidini, kiroho kukawa dhaifu udhibiti wa kidola ndio hatua inayofuatia. Ni jukumu la viongozi kuokoa hali hii ya mtu kujizuia yeye mwenyewe bila shuruti na kuihami hali isije kudharauliwa na kutwezwa.

Moja ya malengo ya Shari'ah ni kuzifanya nyepesi amri zake katika sifa tofauti zinazohimiza hivyo na zinabadilika kutokana na amri mbalimbali. Shari'ah inawahusu watu wote na ni ya milele na mabadiliko ya hali ni sura muhimu katika sheria tukufu kuyazingatia.

Maelezo ya Shari'ah juu ya miamala yana malengo mawili: Wakati mwingine lengo lake ni kuwalazimisha watu na kanuni au hukumu ya kudumu na ya watu wote kama vile kuharamishwa kwa riba. Wakati mwingine lengo lake ni kuhukumu kati ya watu ambapo uamuzi maalumu wa kimahakama unajumuisha utekelezaji wa kanuni ya Shari'ah inayohusu watu wote. Kwa kuwa tunatilia maanani kuziba na

kuzuia njia zinazopelekea katika haramu kama moja ya njia za kanuni kuu za Sheria ya Kiislamu, kwani kanuni yake hufanya kazi chini ya hali maalumu, mujtahiduna lazima wazingatie wakati gani njia hizo lazima zizuiwe au kuzibwa na wakati gani zinaweza kuachwa wazi.

## Lengo la Shari'ah katika Kujenga Mfumo Imara na Madhubuti wa Kijamii

Lengo kubwa la Shari'ah ni kuunda jamii yenye nguvu pamoja na mfumo imara wa kijamii na kuhimiza utendaji mzuri wa mambo yake kwa kuleta manufaa na kuzuia madhara. Tunatakiwa kuichukulia jamii yote ya Kiislamu kama Muislamu mmoja na kuzilazimisha hali zake kwa kanuni za Shari'ah kwa watu wote kama tunavyofanya kwa mtu mmoja mmoja. Vile vile tunahitaji kupata uoni wa wazi kuhusiana na namna hukumu na kanuni za Sheria ya Kiislamu zinavyotakikana zitumike katika mambo ya jamii. Kuzuia njia, kuzingatia maslahi ambayo hayajaainishwa moja kwa moja na dalili za Kisheria, na kanuni ya ruhusa ni sifa muhimu zinazohusu jamii yote na kwa mara chache hutumika kwa mtu mmoja mmoja.



Jukumu la wanazuoni ni kutoa masuluhisho ya Sheria ya Kiislamu kwa matatizo ya jamii. Allah amezikemea jamii nyingi kwa kukubali maana za juu juu tu za mambo pasi na kuangalia kwa undani na kutafuta maana za ndani za mambo. Hivyo hivyo, kufanya ijtihadi ni wajibu wa pamoja wa jamii ya Kiislamu kutokana na mahitaji na hali zao tofauti katika nchi tofauti. Jamii yote ya Kiislamu hupata dhambi kwa kushindwa kutekeleza jukumu hili wakati njia na vitendea kazi vyake vipo.

Madhara hasi ya kushindwa kufanya ijtihadi yanaonekana wazi katika zile sura za maisha ya Waislamu ambazo zimebadilika tangu wakati wa wanazuoni wakubwa waliokuwa wanajitahidi. Waislamu wanahitaji wasomi ambao wanaweza kutathmini na kuchambua rai za madhehebu mbalimbali na kuamua ipi waipe kipaumbele ili jamii yote iwe katika makubaliano. Katika daraja zote hizi kuna hitajio la dharura na muhimu sana la kusoma kwa kina na kujadili Shari'ah katika kupima malengo yao ya awali na upili pamoja na urahisi wa utekelezaji au ugumu wa utekelezaji wa madhehebu ya mujtahiduna wa mwanzo.

Hatua ya kwanza na nyeti ya kuliendea lengo hili muhimu la kisomi ni

kuunda chombo cha wataalamu na wasomi wa Shari'ah kutoka katika mitazamo yote ya kifiqh katika nchi za Kiislamu. Wanazuoni hawa wanatakiwa kuyapitia kwa kina na kujadili mahitaji muhimu ya Ummah wa Kiislamu ili kutoa maazimio waliyokubaliana kwa ajili ya Ummah wote wa Kiislamu. Jukumu lingine muhimu ni kuainisha wanazuoni wa Shari'ah duniani ambao wamefikia daraja ya kufanya ijtihadi. Pamoja na elimu zaidi ili hawa waweze kufikia daraja ya Ijitihadi lazima wawe na tabia njema, wawe na utu na pia watekeleze Shari'ah kwa vitendo katika maisha yao binafsi ili Ummah wa Kiislamu uwe na imani kamili katika elimu yao.

# SEHEMU YA TATU

*Malengo ya Shari'ah:*

*Miamala Ya Kibinadamu*



## Njia na Hatma katika Miamala

Mada hii ni hitajio muhimu kwa ajili ya kupima kanuni za Shari'ah kutoka katika tabia ya mwanadamu na maingiliano ya kijamii. Lengo lake ni kutofautisha kati ya hatma ambazo Shari'ah huwekea kipaumbele kwa ajili ya kutambua na kuzuia kutoka katika njia ambazo zinachukua nafasi ya pili kwa sababu zinategemea juu ya kitu kingine zaidi. Maudhui ya kanuni za Shari'ah yanaangukia katika makundi au mafungu mawili: Hatma na Njia. Hatma au malengo yanajumuisha Maslahi na Mafsada, wakati njia zinajumuisha mifumo inayopelekea katika hatma.

Hatma ni aina za tabia zilizokusudiwa kwa ajili ya manufaa ya wanadamu na zimegawanyika katika matendo kwa mujibu wa malengo ya Allah na zile zilizokuwa zimeasisiwa na malengo ya wanadamu. Malengo ni mbinu zilizokusudiwa na Allah kwa aijli ya kutambua malengo yenye manufaa au kuhifadhi manufaa ya jamii yanayohusiana na tabia binafsi. Aina ya pili ambayo ni muhimu kama ya kwanza na haijaenea kama ya kwanza, inajumuisha malengo yaliyotekelezwa na kikundi maalumu cha watu au mtu mmoja mmoja. Aina mbili hizo za malengo zimegawanyika

zaidi katika haki za Allah na haki za wanadamu. Asili ya haki hizi iko katika namna ambayo hakuna yeyote anayeruhusiwa kuzidhararu kwa sababu ni njia ya kulinda malengo makuu na ya mwisho ya Shari'ah.

Neno "Wasaail" humaanisha kanuni alizoweka Allah kama njia ya kutambua malengo ya muda na kama njia zinazopelekea katika malengo ya mwisho. Bila hayo lengo la Shari'ah linaweza kukosekana moja kwa moja au yanaweza yasipatikane au yasipatikane yote. Njia zinajumuisha sababu zinazoonesha kanuni za Shari'ah, masharti muhimu kwa ajili ya utekelezaji wao, na kukosekana vizuizi. Hii ndiyo sababu imekuwa ni kanuni kuu za fiqh kuwa kama lengo likibatilishwa, ni hivyo hivyo na njia lazima zibatilishwe. Mjadala huu unahusu njia zinazotakikana katika kuyatambua malengo ya Shari'ah.

## Kanuni na Aina za Haki Katika Shari'ah

Kuainisha kanuni za kumiliki ndiyo mazingira mazuri na imara zaidi ya kuiwekea sheria na kanuni miamala ya watu ili kutimiza malengo mawili muhimu ambayo ni msingi wa kutoa haki kwa wahusika. Kuweka kanuni hizo kunaimarisha na kuelezea na kuweka wazi haki za majaji, viongozi na watetezi.



Lengo kuu la Shari'ah ni kuainisha haki tofauti kulingana na makundi mbalimbali ya watu wanaohusika pamoja na kupima endapo baadhi ya watu watapewa kipaumbele juu ya watu wengine katika haki fulani na kuonesha namna watu wanavyotakiwa kugawana manufaa ya rasilimali ambazo zinatakiwa wagawane.

Umuhimu wa kuainisha kanuni zinazotawala haki mbalimbali unaweza kuonekana katika kanuni kuu mbili za msingi: silka au haki za kuzaliwa nazo, hali ya kutamalaki, au kipaumbele kwa mtu mmoja mmoja dhidi ya mwingine au baadhi ya watu dhidi ya watu wengine katika haki fulani ambazo zinadhulumika kwa urahisi. Haki zinaweza kugawanywa katika makundi haya kwa mujibu wa uzito wa sababu zao zikiwemo haki za msingi za kuzaliwa, haki za utambulisho wa nasaba na haki ya kupata rasilimali.

Mifumo tofauti ya sheria inasisitiza juu ya kanuni inayohusu msingi wa familia ili kuhifadhi na kulinda vizazi kutoka na wasiwasi wa utambulisho wao wa kifamilia. Ikiwa juu ya sheria zote za kweli, Sheria

ya Kiislamu imeweka kanuni au hukumu za uadilifu sana, zenye nguvu sana, na zenye kutukuza sana kwa ajili ya kurekebisha na kufanya kazi kwa familia. Kanuni muhimu kuliko zote inayohusu sheria yoyote inayohusu familia inatakikana ilenge katika kuimarisha ndoa na familia na ifafanue wazi namna ya kuvunja mahusiano haya kama itatokea yakavunjika. Moja ya malengo muhimu sana ya Shari'ah ni kuhimiza ndoa kwa sababu inaunda kanuni ya msingi ya familia.

Mfumo wa mkataba unaotakiwa kuimarisha ndoa katika namna bora zaidi ni kiambata cha msingi wa ndoa. Uchambuzi wetu juu ya vitu vinavyojumuisha kanuni za mwanzo na za pili zinazorekebisha ndoa, na kutohoa malengo ya Shari'ah yanayohusu ndoa yanaweza kutoholewa na kutuwezesha kufuatisha kanuni mbili kuu muhimu. Kanuni ya kwanza inalenga katika kuanzisha tofauti ya wazi kati ya muundo maalumu wa ndoa na miundo mingine ya mahusiano kati ya mwanamke na mwanamme. Kanuni ya pili inajumuisha kuhakikisha ndoa haifungwi katika msingi wa muda. Ndoa ni mfumo wa kulinda na kuhifadhi maadili.



## Miamala

Shari'ah ya Kiislamu ina angalizo la juu sana kuhusiana na utajiri wa kiuchumi. Aya za Qur'an na Hadithi za Mtume zinaongelea utajiri kama msingi wa shughuli za jamii na utatuzi wa matatizo yake. Kuna dalili za Kishari'ah ambazo ni ushahidi wenye nguvu kuwa mali na utajiri vina nafasi muhimu kutokana na Shari'ah. Zaka imefaradhishwa juu ya mali na ni nguzo ya tatu ya Uislamu. Lengo kuu la Shari'ah juu ya mali ya jamii ni kuhakikisha uihifadhi na ukuzi wake.

Shari'ah imetaja vitu vifuatavyo kama njia pekee za kupatia: umiliki wa kitu ambao mtu mwingine hana haki; mtu kukifanyia kazi kipande cha ardhi pamoja na mmiliki wake na kubadilishana kitu kimoja kwa kingine. Soko humaanisha mzunguko wa mali wa haki katika mikono ya idadi ya watu wengi kadiri iwezekanavyo. Kwa hiyo unajumuisha kusudio moja kubwa la Shari'ah. Kupata lengo la soko, mikataba inayohusu aina mbalimbali za miamala imewekwa ili kurekebisha uhamishaji wa haki za kifedha. Malengo ya Shari'ah yanayohusu aina zote za uchumi yanaweza kufupishwa chini ya soko, uwazi, uhifadhi, umadhubuti na usawa.

Moja ya maana za mzunguko unaokusudiwa na Shari'ah ni uhamishaji wa mali ndani ya jamii katika mikono mingi kadiri iwezekanavyo pasipo kusababisha madhara yoyote kwa wale walioipata kwa njia ya halali. Shari'ah inakiri haki ya umiliki binafsi wa mali na imewaruhusu wamiliki kuitumia mali hiyo kihalali kama wanavyopenda wakati wa maisha yao. Kwa kufanya hivyo Shari'ah inahamasisha kuchuma na kuhifadhi mali. Kwa njia hii Shari'ah inatumai kulifikia lengo lake la kuongeza mali ya ujumla ya jamii na kuondosha vikwazo vya kuendelea kwa jamii kiuchumi.

Lengo la kuhitajia uwazi katika mali na bidhaa ni kwa ajili ya kuzuia madhara na ugomvi kwa kadri iwezekanavyo. Hii ndiyo sababu ambayo kupitia kwayo mikataba na udhibiti wake katika mfumo wa nyaraka imefaradhishwa. Yeyote yule aliyepewa dhamana ya aina yoyote ya mali ni lazima ailinde kwa mujibu wa maamrisho ya Allah. Kanuni za Shari'ah zinatawala kukubalika na kusahihishwa kwa mikataba na kutimiza masharti yake.

Ni kutokana na kuendana na lengo la Shari'ah linalohusu miamala ya kifedha kanuni zinazotawala uhalali au uharamu wa mikataba inayohusiana na umiliki na upataji wa mali imewekewa sheria. Lengo la Shari'ah katika aina tofauti za miamala ya kifedha ni kumwezesha mtu mmoja mmoja na jamii kupata mali. Wafanyakazi ni moja ya nyezo za msingi za kupatia mali.



Watu wenye uwezo wa kufanya kazi na uzalishaji mali wengi wao hawana mtaji wenye kuwawezesha kufanya shughuli za uzalishaji au hawana mtaji wa kutosha unaoendana na uwezo wao wa uzalishaji. Mtaji na wafanyakazi ni vitu ambavyo vinaweza visiwekwe katika matumizi ya uzalishaji katika mambo mengi. Hali hii huchangia hasara kubwa kwa wafanyakazi, wamiliki wa mtaji na jamii yote kwa ujumla.

Kuondoa hali hii, watu wenye fikra sahihi wanaelekezwa kugundua njia za kujumuisha mtaji na wafanyakazi wenye ujuzi ili kunufaisha pande zote mbili. Kwa hiyo ni lengo kuu la Sheria ya Kiislamu kutozuia moja ya viwili hivi katika kufuata njia nzuri zaidi za kupata au kufikia lengo hili kwa njia ya uadilifu. Lengo la Shari'ah katika aina zote hizi za mikataba ni kulinda haki za wafanyakazi kwa kuweka masharti maalumu ili kazi zao zisipotee bure au zisienziwe na kuthaminiwa.

Shari'ah inaunga mkono kanuni zifuatazo: Kuongeza mikataba yenye msingi wa vibarua; kuruhusu uthubutu ambao ni wa kawaida kwa biashara zinazofanana; kuzuia chochote kile ambacho humuelemea mfanyakazi katika mikataba hiyo pasi na kuzingatia kuwa mikataba ina nguvu za kisheria kivitendo; kuruhusu sheria ya kuwapa wafanyakazi malipo zaidi ya yale wanayopata kwa mujibu wa kazi walizofanya, kuwalipa wafanyakazi malipo yao mara tu wamalizapo kazi zao pasipo kuwacheleweshea, kuwapa wafanyakazi njia au nyezo za kukamilisha kazi zao maana hawatakiwi kulazimishwa kumaliza kazi wenyewe ikiwa zipo nje ya uwezo wao; na kuondosha aina zote za masharti yanayofanana na kazi za watumwa. Zawadi na mikataba ya michango imejengwa katika wazo la kusaidiana miongoni mwa wanajamii. Inaimarisha udugu na kuakisi malengo makuu ya Shari'ah na kuwakilisha utukufu wa Shari'ah.

Vile vile inasaidia wenye matatizo na umasikini. Shari'ah inaunga mkono kanuni zifuatazo: Kuongeza michango na zawadi kwa mtazamo wa maslahi binafsi na maslahi ya jamii; michango ya hiari na isiyoambatana na kulazimisha; uvumilivu na unyumbufu vinavyotumiwa katika njia za kuhalalisha mikataba ya michango kutokana na matakwa ya watoaji; na kitendo cha kuchangia kisipelekee katika kuvunja na kukosesha haki za watu wengine.



## Ujaji, Ushahidi Na Adhabu

Jamii ya Kiislamu inatakikana iwe na viongozi wanaoendesha mambo yao ya kijamii, wanaotenda haki na kutekeleza hukumu za Shari'ah katika ngazi mbalimbali. Hii ni kwa sababu Sheria ya Kiislamu pamoja na kuwa ni mfumo wa kutawala mahusiano ya watu na kuwapa haki iliteremshwa ili kufikia malengo haya tu. Moja kati ya malengo makubwa kabisa ya Shari'ah baada ya kuielezea ni uanzishwaji wa mamlaka yake, utekelezaji wa hukumu zake, na kulingania ukuu wake.

Kuhakikisha utekelezaji wa mfumo wowote ule wa sheria; watu wanatakikana kwa kiasi kikubwa sana wawe wamejazwa hisia ya utukufu wa Sheria hiyo. Kwa hakika watu waliopata kukinaishwa juu ya uzuri na ubora wa sheria huweza kuitii bila shuruti.

Malengo ya Sheria kwa wahusika na utekelezaji wa hukumu zake vimewekwa ili kutoa haki kwa walalamikaji wa kweli kwa mujibu wa

kanuni kuu na kanuni maalumu. Yeyote aliyechaguliwa katika ofisi yototе jukumu lake ni kuleta manufaa na kuzuia madhara kwa watu. Shari'ah inalenga katika kuboresha hali ya jamii katika mambo yake yote. Onyo, adhabu, na adhabu maalumu zilizowekwa na Shari'ah zinalenga kwa ujumla wake kurekebisha hali za watu. Moja ya malengo makuu ya Shari'ah ni kulinda na kuhifadhi mfumo wa jamii. Ni kupitia kuzuia na kuziba myanya na vyanzo vya misuguanao na dhuluma ndipo lengo hili litafikiwa.

Kuziba vyanzo hivi itakuwa ni sera nzuri pale tu hili litakapoasisiwa katika msingi wa sheria tukufu na ikatekelezwa na mamlaka halali ya Kisheria. Kuwabadilisha watu na jamii ni lengo kubwa kuliko malengo yote ya Shari'ah. Sheria ya Kiislamu inalenga katika kuleta ridhaa kwa wahanga kukosewa kwa kupitia mfumo wa kuwaadhibu wakosaji na kuwakanya waigaji.

## Hitimisho

Inatarajiwa kitabu hiki kitawafaa wanazuoni wa Fiqh na watafutaji wa elimu ya kina katika kunyanyua kwa daraja ya juu kabisa fikra zao na utambuzi wao na kuimarisha azma yao ya kufuata na kupata Makusudio Makubwa ya Shari'ah.

# KUHUSU MTUNZI

Muhammad Al-Tahir Ibn Ashur alizaliwa Tunisia mwaka 1879 na alifariki 1973. Ameacha hazina ya uzoefu mkubwa na wa muda mrefu katika maisha ya kijamii na kiutawala pamoja na urithi mkubwa wa machapisho na makala za kitaaluma zisizo na mfano wake katika Tunisia ya karne ya kumi na tisa na karne ya ishirini; mengi ya machapisho na makala bado hazijasomwa kwa kina na kuchapishwa.

Sheikh Muhammad al-Tahir Ibn Ashur ni Imamu maarufu na ni miongoni mwa wanachuoni wakubwa wa Kiislamu wa karne ya 20. Kitabu hiki cha makala ya Sheikh Ashur kuhusu Makusudio ya Sharia ni katika mafanikio makubwa ya kusoma Sharia ya Kiislamu kwa lugha ya Kiswahili.

Katika kitabu hiki, Sheikh Ibn Ashur amependekeza 'Makusudio' kama mbinu ya kuijenga upya nadharia ya Sharia ya Kiislamu ambayo haikuendelezwa ipasavyo tangu kughibu kwa maimamu wakubwa. Amejadili suala nyeti la makusudio ya vitendo vya Mtume (s.a.w) na maamuzi yake, na ameweka vigezo vya Hadithi za Mtume zilizo kusudiwa kuwa sehemu ya Sharia na vitendo vya Mtume (s.a.w) vilivyofungamana na malengo maalumu ya kuongoza siasa na kutatua migogoro. Mchango mkubwa aliotoa Sheikh Ibn Ashur katika kitabu hiki ni kuunda nadharia mpya ya 'makusudio' kwa kuleta istilahi mpya ambazo kabla hazikuwepo katika misingi ya fiqhi ya kale.

MUHAMMAD AL-TAHIR IBN ASHUR

IIIT — Mfululizo wa Vitabu kwa Muhtasari